# WANAWAKE na ARDHI

Ardhi ni Uhai

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

TOLEO LA 4

MACHI 2021

# NANI ATETEE HAKI ZA WANAWAKE WA VIJIJINI KUMILIKI ARDHI?

*Na Iringa Civil Society Organization (ICISO – UMBRELLA)*

Nani atetee haki za wanawake katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi? Hili ni swali ambalo limekuwa likiibuka katika mijadala na mafunzo ya Sheria za Ardhi na haki za ardhi kwa wanawake kwenye maeneo mengi nchini. Msingi wa swali hili ni kuwa mara nyingi inaonekana kuwa watetezi wa haki za wanawake hususani wale wanaoishi vijijini ni watu wengine kutoka mijini. Je, ni kweli kuwa wanawake wa vijijini na pembezoni mwa miji hawana uwezo wa kutetea haki zao?

Swali hili linajibiwa na Bi. Rehema Salum Ngwada ambaye ni Katibu wa Jukwaa la Wanawake katika Kijiji cha Mgowelo kilichoko Wilayani Kilolo, Mkoa wa Iringa. Kwa mujibu wa Bi. Rehema yeye pamoja na dada zake hawakupewa ardhi katika familia yao kutokana na mila na desturi ambazo hazimruhusu mtoto wa kike kumiliki ardhi kwa wazazi wake kwa sababu tu ataolewa na ataenda kupata ardhi kutoka kwa mume wake.

*Inaendelea uk. 4*



YALIYOMO

- NAFASI YA SANAA KATIKA UTETEZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE — 5
- UMILIKI WA ARDHI NI AHUENI KWA WANAWAKE — 6
- FAHAMU UMUHIMU WA MABARAZA YA ARDHI YA VIJIJI KWA WANYONGE — 7
- VIJANA WANA NAFASI YA UJUMBE KATIKA MABARAZA YA VIJIJI NA KATA — 8-9
- NGUVU YA MWANAMKE NI UKOMBOZI WA FAMILIA — 9-10
- HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE NA MAENDELEO YA KIUCHUMI — 11-12
- MAJUKWAA YA WANAWAKE DARAJA LA MATUMAINI VIJIJINI — 12-13
- JAMII IBADILI MTAZAMO KUHUSU HAKI ZA WATOTO WA KIKE — 13-14
- TABASAMU LILILOFIFISHWA LACHOMOZA TENA — 14-15



Cathbert Tomitho
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Utafiti na
Utetezi wa Haki za Ardhi.

# WANAWAKE na ARDHI

Hili ni toleo la nne la Jarida la Wanawake na Ardhi lililosheheni makala zinazohusu mafanikio na changamoto zinazowakabili wanawake katika upatikanaji, utumiaji na umiliki wa ardhi nchini Tanzania. Makala hizi zinatokana na matokeo ya utekelezaji wa mradi wa haki za ardhi kwa wanawake unaotekelezwa na asasi kumi na mbili za kiraia zinazounda Kongani ya Haki za Ardhi kwa Wanawake. Asasi hizi ni HAKIARDHI, WEMWA, TARWOC, WODSTA, UMWEMA, TAWLA, CEDESOTA, ICISO, AVCD, MPLC, UCRT na COSITA. Wilaya ambazo mradi huu unatekelezwa ni Kiteto, Iringa vijijini, Morogoro vijijini, Kilolo, Arusha vijijini, Meru, Manispaa ya Singida, Mufindi, Kilosa na Babati. Mradi huu unafadhiliwa na shirika la Foundation for Civil Society tangu mwaka 2017.

Kwa ujumla makala zilizomo katika Jarida hili zimeangazia masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwezo walio nao wanawake wa vijijini na pembezoni mwa miji katika kutetea haki zao pasipo uhitaji wa wadau wengine walioko mijini; Vile vile, nafasi ya sanaa katika kufikisha elimu ya haki za ardhi nayo imegusiwa kwa kina; umuhimu wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata katika kutenda haki kwa makundi yote katika jamii; Nafasi ya vijana katika Mabaraza ya usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya ardhi; Jamii kuachana na mitizamo hasi kuhusu mtoto wa kike katika kupata elimu na kumilikishwa mali ikiwa ni pamoja na ardhi; Pamoja na makala hizi kuna makala nyingine kede kede zitakazompa msomaji nafasi ya kufahamu kazi kubwa inayofanywa na asasi za kiraia kwa kushirikiana na Serikali katika ngazi ya Wizara, Halmashauri za Wilaya pamoja na Halmashauri za Vijiji.

Tukiwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021 tumeshuhudia matukio ambayo yametengeneza kumbukumbu katika historia ya nchi yetu, asasi za kiraia na jamii kwa ujumla. Tukio kubwa na la kuhuzunisha ni kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyefariki Machi 17, 2021. Msiba huu ulilishtua Taifa kutokana na uzalendo aliokuwanao Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa Taifa na wananchi wake kutokana na maamuzi mbalimbali ya kimaendeleo aliyoyatekeleza wakati wa uongozi wake. Katika sekta ya ardhi Hayati Dkt. John Pombe Magufuli atakumbukwa kwa mengi ikiwa ni pamoja na kufuta hati za mashamba yasiyoendelezwa na kuagiza yagawiwe kwa Wakulima na Wafugaji wenye uhitaji wa ardhi ya kilimo na ufugaji; Kushughulikia migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji na kuridhia uamuzi wa kuvirasimisha vijiji 920 kati ya 975 ambavyo vilitakiwa kufutwa kwa madai kuwa vipo ndani ya maeneo ya hifadhi; pamoja na kusisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika usikilizwaji wa kesi na uandishi wa hukumu ili wananchi wasipoteze haki zao kwa kigezo cha kutokufahamu lugha ya Kiingereza ambayo imekuwa ikitumika kwa miaka mingi.

Vile vile, mwezi Februari 2021 sekta ya asasi za kiraia nchini ilipata pigo kubwa kutokana na kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi wa MPLC Bi. Flora Massoy. Hayati Bi. Flora alikuwa miongoni mwa wanaharakati wa kwanza na nguli katika utetezi wa haki za wanawake nchini. Hayati Bi. Flora ameshiriki katika kufanikisha mabadiliko ya sera na sheria mbalimbali kwa lengo la kutetea utu na haki ya mwanamke katika jamii ya Kitanzania. Hayati Bi. Flora atakumbukwa sana na wanawake wa vijijini kutokana na kusimama kidete katika kuhakikisha kuwa wanafahamu wajibu wao katika kutetea haki zao. Ni dhahiri kuwa mchango wa Hayati Bi. Flora utakumbukwa siku zote popote pale zinapotajwa haki za wanawake.

Halikadhalika, Machi 19, 2021 tulishuhudia kuapishwa kwa Rais wa kwanza mwanamke nchini Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili ni tukio kubwa sana sio tu kwenye historia ya Taifa letu bali katika ukanda wote wa Afrika Mashariki kwa sababu ndiye mwanamke wa kwanza kuwa Rais. Sisi kama wadau wa haki za ardhi kwa wanawake tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza majukumu yake pamoja na kutumia uwepo wake madarakani kama fursa ya kuhakikisha kuwa haki za wanawake na watoto wa kike zinalindwa sio tu katika sekta ya ardhi lakini katika sekta zote.

Kama ilivyo ada ya kila mwaka tarehe 8 Machi huwa ni maadhimisho ya siku ya wanawake duniani. Kwa mwaka 2021 ujumbe mahsusi wa siku hii ulikuwa ni "Wanawake katika uongozi chachu ya kufikia dunia yenye usawa." Rai yetu kama wadau wa masuala ya ardhi ni kuitaka serikali serikali iimarishe mifumo ya kisheria na kitaasisi itakayowawezesha wanawake hususani waliopo vijijini kunufaika na ardhi na rasilimali nyinginezo. Kwa tafsiri nyepesi ni kuwa wanawake wapewe kipaumbele cha kuwa wawekezaji katika ardhi za vijiji kwa kuwa ndio wazalishaji wakubwa. Hili linawezekana kwa Serikali kuimarisha miundombinu na masoko ambayo wanawake watauza mazao wanayovuna ili wapate faida watakayowekeza katika uzalishaji zaidi. Ni muhimu pia kwa Serikali kusimamia mabenki yatakayowakopesha wanawake pasipo kuwanyonya kupitia mikopo yenye riba kubwa.

Mwisho, niwatakie usomaji mwema wa makala zilizomo katika Jarida hili. Kwa maoni ya kuboresha Jarida letu usisite kuyawasilisha kupitia barua pepe ambayo ni info@hakiardhi.or.tz au simu ya bure namba 0-800-711-555. Unaweza pia kupata machapisho zaidi kwa kutembelea tovuti ambayo ni www.hakiardhi.or.tz pamoja na mitandao ya kijamii ya Facebook, Twitter na Instagram.

ARDHI NI UHAI



# HUYU NDIE MJANE JASIRI ALIYETETEA HAKI YAKE PASIPO WOGA

*Na Community Economic Development and Social Transformation (CEDESOTA)*



*Bi. Josephine aliyefanikiwa kurejesha shamba lake alilokuwa amedhulumiwa*

Ujasiri ni asili ya kila binadamu aliyeumbwa na Mwenyenzi Mungu tofauti pekee ni namna gani kila binadamu anavyotumia ujasiri alionao kwenye maisha yake ya kila siku. Wakati mwingine tafsiri ya ujasiri imekuwa ikitofuatiana kutoka tukio moja hadi jingine. Ingawa mara nyingi mtu anayetunukiwa sifa ya ujasiri ni yule anayetenda mambo chanya kwenye familia yake, jamii yake, kijiji chake, kazi yake au taifa lake. Ni nadra sana mtu anayefanya mambo maovu kupata nishani hii ya ujasiri.

Moja ya watu waliofanikiwa kupata nishani ya ujasiri ni Mjane anayetambulika kwa jina la Bi. Josephine Cleopa Mafieni. Mjane huyu ni mkazi wa Kijiji cha Leguruki Wilaya ya Meru, akijishughulisha na kazi za kilimo na ufugaji. Katika kupambana na ugumu wa maisha Bi. Josephine aliuza kuku na mbuzi wake kwa lengo la kununua eneo la ardhi lenye ukubwa wa robo ekari kwa gharama ya shilingi Laki Moja na Ishirini Elfu tu (120,000/=). Katika hali ya muuzaji wa eneo hilo aliliuza tena kwa mara ya pili kwa mtu mwingine aliyefahamika kwa jina la Ndugu Eliakesia Jeremia.

Sababu ya kuuzwa shamba kwa mara ya pili ni kutokana na namna mwanamke hususani Mjane anavyotafsiriwa katika jamii kuwa ni kiumbe dhaifu, asiye na maamuzi na asiyeweza kujitetea mbele ya mwanaume. Kwa maana hiyo muuzaji alifikiri na kuamini kuwa Bi. Josephine kwasababu ni Mjane asingeweza kutetea haki yake popote.

Wakati Bi. Josephine akiwa katika harakati za kutafuta namna anavyoweza kukomboa ardhi yake alifanikiwa kupata fursa ya kushiriki kwenye mafunzo ya sheria za ardhi na haki za ardhi yaliyokuwa yanatolewa na taasisi ya CEDESOTA. Katika mafunzo hayo ndipo Bi. Josephine alipojifunza mambo mengi kuhusiana na haki za wanawake katika kumiliki ardhi. Vilevile, aliweza kufahamu vyombo vya kisheria ambavyo angeweza kupeleka kesi yake ili aweze kutetea haki yake. Baada ya mafunzo hayo Bi. Josephine alipeleka kesi yake katika Baraza la Ardhi la Kijiji.

Bi. Josephine anasema kuwa baada ya kupeleka kesi kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji na baada ya kusikilizwa lilihamishiwa katika Baraza la Kata. Baraza la Kata lilitoa hukumu ambayo ilimtaka mlalamikiwa kurudisha eneo langu pamoja na kutakiwa kulipa gharama zote za kesi kutokana na usmbufu aliousababisha.

Bi. Josephine anaongeza kwa kusema kuwa amefurahi sana kupata eneo lake ambalo analitumia katika uzalishaji mali ikiwemo kulima mazao yanayomsaidia kulisha familia yake na mengine kuuza na kujipatia kipato kinachomsaidia kutunza watoto wake.

›› Inatoka uk. 1

Bi. Rehema anaendelea kueleza kuwa yeye na dada zake waliridhika na kutokupewa ardhi kwa sababu walifahamu ndio mila na desturi zao na sio wao tu wamenyimwa ardhi bali hata katika familia nyingine za ndugu zao na majirani wamekuwa wanaona namna ambavyo watoto wa kike hawarithishwi ardhi.

Bi. Rehema anaeleza kuwa alishangaa sana siku moja mwezi Julai 2019 alipopata nafasi ya kushiriki mafunzo ya Sheria za Ardhi na haki za ardhi yaliyokuwa yanatolewa na shirika la ICISO na kusikia kuwa kwa mujibu wa sheria wanawake wana haki sawa na wanaume katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi. Kwa mjibu wa Bi. Rehema anasema hakuamini masikio yake pale mtoa mafunzo aliposema kuwa watoto wa kike wana haki ya kurithi ardhi kutoka kwa wazazi wao sawa sawa na watoto wa kiume.

Bi. Rehema anasema kuwa punde tu baada ya mafunzo yale alianza kufuatilia haki yake ya kupata na kumiliki ardhi kutoka kwa wazazi wake. Anasema kuwa katika kufuatilia haki yake alianza kwa kuwaelimisha wazazi na kaka zake ambao ndio walikuwa wamemilikishwa ardhi yote. Bi. Rehema anasema kuwa Mungu alimsaidia sana kwa sababu wazazi na kaka zake walimuelewa na ilipofika mwishoni mwa mwaka 2020 alifanikiwa kupata ekari 2 za shamba pamoja na ng'ombe 4. Vile vile, dada zake wawili nao walipata ekari 2 kila mmoja. Kwa sasa Bi. Rehema na dada zake wanaendelea kufuatilia hati miliki za mashamba yao. Bi. Rehema anaongeza kwa kusema kuwa;

***"……..kufanikiwa kwangu na dada zangu kupata mali kumechangiwa na elimu inayotolewa na shirika la ICISO, awali wazazi wangu na kaka zangu hawakuona umuhimu wowote wa sisi watoto wa kike kumilikishwa ardhi na mali. Elimu hii imerahisisha mambo kwa sababu wazazi, mimi na kaka zangu tulihudhuria kwenye mikutano na waliisikia vizuri elimu ya usawa katika umiliki wa mali na ardhi."***



*Bi. Rehema Salum Ngwada kutoka kijiji cha Mgowelo Wilayani Kilolo*

Wito wa Bi. Rehema kwa wanawake wenzake na jamii yote husussani wale wanaoishi vijijini ni kuhakikisha kuwa wanachukua wajibu wa kutetea haki zao kwa sababu hakuna mtu mwingine atakayefanya hivyo vizuri zaidi ya yule anayenyanyasika. Vilevile, Bi. Rehema anaiasa jamii kuwa wazazi wanapofanya maamuzi ya kugawa ardhi kwa watoto wao basi mgao uzingatie usawa kwa watoto wa kike na kiume badala ya kugawa kwa watoto wa kiume pekee kwa kuwa watoto wa kike pia wana haki ya kumikishwa ardhi kutoka kwa Wazazi wao.

# NAFASI YA SANAA KATIKA UTETEZI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE

*Na Community Support Initiatives – Tanzania (COSITA)*



*Bi. Fatina akiwa amesimama mbele ya nyumba yake wakati ikifanyiwa marekebisho*

Uelewa mdogo wa haki za wanawake hasa kumiliki ardhi umekuwa ndio chanzo cha unyanyasaji katika jamii nyingi nchini Tanzania. Wanawake wengi husussani wanaoishi vijijini hunyang'anywa mali zao kutokana na kutokujua sheria zinazowapa fursa ya kumiliki mali ikiwemo Sheria za Ardhi Na. 4 na 5 za mwaka 1999 zinazowapa haki ya kumiliki ardhi. Taasisi ya COSITA katika utekelezaji wa shughuli za mradi wa haki za ardhi kwa wanawake katika Wilaya ya Babati hutumia kikundi cha sanaa cha DUMA katika kuielimisha jamii kuhusu haki za mwanamke katika ardhi na rasilimali zingine.

Kikundi cha DUMA kilijengewa uwezo kuhusu Sheria na haki za ardhi kwa wanawake, elimu hii iliwawezesha wana kikundi kuandaa nyimbo na maigizo yaliyobeba jumbe mbalimbali kuhusu haki za ardhi kwa wanawake kwa lengo la za kuhamasisha jamii katika ngazi za vijiji.



*Bi.Fatina akiwa mbele ya nyumba yake baada ya kufanyiwa marekebisho.*

Katika utekelezaji wa kazi zake kikundi cha DUMA kwenye vijiji vya Babati walikutana na mwanamke mjane aitwaye Bi. Fatina Omary Chokay (67), mkazi wa Babati ambaye nyumba yake ilinusurika kuuzwa na binti yake aitwaye Bi. Arafa Said Sariko baada ya nyumba hiyo kufanyiwa maboresho na kuongezeka thamani. Wanakikundi walimpatia elimu Bi. Fatina ya namna ya kufuatilia haki yake ya kunusuru nyumba yake isiuzwe kinyemela na Binti yake. Pamoja na kumpatia elimu vilevile walimpatia machapisho yaliyokuwa yanaeleza utaratibu wa kisheria wa kufuatilia haki yake kama mwanamke na kama mwananchi mwingine yeyote.

Katika ufuatiliaji wa haki yake Bi. Fatina alifanikiwa kwenda hadi kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Ndugu Alexander Mnyeti kupeleka lalamiko lake na baada ya kumsikiliza kwa makini alitoa maagizo kuwa binti arudishe fedha za mtu aliyetaka kununua nyumba hiyo na Mama arejeshewe nyumba yake kwa kuwa ni mali yake halali aliyoachiwa na marehemu mume wake. Katika mahojiano baina ya COSITA na Bi. Fatina alisema mambo yafuatayo;

***"…..kwa sasa nina furaha kwa sababu ninaishi kwa amani katika nyumba yangu pia nawashukuru Mkuu wa Mkoa pamoja na vijana wa kikundi cha sanaa cha DUMA kwa kuhakikisha wananishika mkono na kupata haki yangu…."***

Anasema Bi. Fatina

# UMILIKI WA ARDHI NI AHUENI KWA WANAWAKE

*Na Morogoro Paralegal Centre (MPLC)*



*Mkuu wa Idara ya Ardhi kutoka Halmashauri ya Wilaya Morogoro, Ndugu Patrick Mwakilili akimkabidhi hatimiliki ya kimila mkazi wa Kijiji cha Gomero, Bi. Tatu Maleta.*

Kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 mtu, kundi la watu na taasisi inaruhusiwa kumiliki ardhi kwa kupewa cheti cha hakimiliki ya Kimila. Cheti hicho hutolewa na Halmashauri ya Kijiji. Umiliki wa ardhi umekuwa na nafuu kubwa kwa wanawake ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi ya kuboresha maisha yao ya kiuchumi kwa kuendeleza kilimo pasipo wasiwasi wowote. Vilevile, umiliki huu wa ardhi hupunguza na kuepusha migogoro ya ardhi ya mara kwa mara baina ya watumiaji wa ardhi. Watalaamu wa masuala ya mipango ya matumizi ya ardhi husema kuwa ardhi inapomilikiwa kwa mujibu wa sheria inasadia kwa kiwango kikubwa katika kubadili taswira ya eneo.

Kituo cha Wasaidizi wa Kisheria Morogoro (MPLC) ni miongoni mwa taasisi zilizojikita kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa kutoa mafunzo ya sheria za ardhi pamoja na kuhamasisha wananchi kumiliki ardhi kisheria kwa kuzingatia matumizi bora na endelevu ya ardhi katika uzalishaji mali ili kujipatia maendeleo.

Bibi Amina Abdallah Fundi mwenye umri wa miaka 81 ni mkazi wa Kijiji cha Gomero ambaye alifika kijijini hapo mwaka 1974 na kupewa eneo na Halmashauri ya Kijiji kwa matumizi ya makazi pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi. Mwaka 1979 Bi. Amina alifiwa na mumewe Bw. Abdallah Fundi na kumuacha na watoto 2. Bi. Amina aliendeleza makazi yake ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba ya kudumu katika eneo hilo.

Kwa sasa Bibi Amina amepima eneo lake lenye ukubwa wa ekari moja kwa ajili ya kupata hatimiliki ya kimila. Pia anaendelea na mchakato wa kujenga nyumba nyingine ya kuishi yenye vyumba 3 kwa fedha anazozipata kwenye shughuli zake za kilimo. Bibi Amina anasema kuwa aliamua kupima eneo la shamba lake baada ya kuona kuna migogoro mingi ya ardhi inatokea ndani ya kijiji chao ambayo wakati mwingine kupelekea watu kushindwa kuelewana. Baada ya kusikia tangazo na elimu kutoka kwa wahamasishaji wa masuala ya ardhi ndipo aliamua kupima ardhi yake.

***"...napenda nimiliki eneo langu kisheria kwa sababu nikiwa na hatimiliki sio rahisi mtu kuvamia eneo langu, hivyo nawashauri wananchi kujitokeza kupima maeneo yao ili kuondokana na migogoro ya ardhi"***

anasema Bi. Amina.

# FAHAMU UMUHIMU WA MABARAZA YA ARDHI YA VIJIJI KWA WANYONGE

*Na Community Support Initiatives – Tanzania (COSITA)*



*Elizabeth (aliyebeba mtoto) na Gabriel (aliyesimama) wakiwa mbele ya nyumba waliyoachiwa na wazazi wao pamoja na shamba ambalo limezunguka nyumba*

Katika jamii nyingi nchini Tanzania ni jambo la kawaida kwa migogoro ya umiliki wa mali kuibuka kwenye familia pindi Baba wa familia anapofariki au pale wazazi wote wawili wanapofariki dunia. Uzoefu unaonesha kuwa migogoro hii huibuliwa na ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu huku waathirika wakubwa wakiwa ni watoto wa marehemu ambao huwa wanakosa mwongozo wa nini wafanye ili kutopoteza mali za wazazi wao. Hii tafsiri yake ni kuwa watoto hawa mara nyingi hukosa mtu wa kuwasimamia au kukosa uwezo wa kujisimamia wenyewe hufikia hatua ya kupoteza haki ya kumiliki mali.

Katika kutekeleza kazi zake katika mradi wa haki za ardhi kwa wanawake taasisi ya COSITA ilikutana na watoto wawili yatima ambao ni Elizabeth Gerald na Gabriel Gerald wa Kijiji cha Kiongozi, Wilaya ya Babati ambao chupuchupu wanyang'ang'anywe shamba waliloachiwa na marehemu wazazi wao. Historia ya eneo hilo inaonesha kuwa wazazi wa watoto hawa walipokuwa hai kulifanyika mauziano ambayo kipande cha eneo lenye ukubwa wa mita 17 upana na 20 kwa urefu kiliuzwa kutoka kwenye eneo la jumla lenye ukubwa wa robo tatu ekari linalomilikiwa na familia.

Katika hali ya kushangaza punde tu baada ya wazazi wa watoto hawa kufariki ulifanyika udanganyifu kwa kubadilisha hati ya mauziano na kusomeka kuwa eneo lote la ardhi liliuzwa na wala siyo sehemu ya eneo kama ambavyo hati ya mauziano ilionesha hapo awali.

Shauri hili lilifika katika Baraza la Ardhi la Kijiji na lilisikilizwa mara kadhaa ili kuweza kujiridhisha na taarifa za pande zote mbili. Baada ya mashauriano ya muda mrefu ya kusuluhisha mgogoro huu Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji liliwapatia haki wale watoto baada ya kugundua kwamba kuna udanganyifu umefanyika katika yale mauziano.

Nini kilichowawezesha Wajumbe wa Baraza la Kijiji kuamua walivyoamua? Maamuzi ya Baraza hili yalichagizwa na elimu ya haki za ardhi ambayo wajumbe wa Baraza hili walipatiwa kutoka taasisi ya COSITA. Kwa mujibu wa COSITA kabla ya mafunzo kufanyika kwa wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji walibaini kuwa wajumbe wake walikuwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu haki za wanawake na watoto katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi. Ingawa, baada ya mafunzo wajumbe hawa walionesha hari ya kutenda haki kwa mujibu wa taratibu za kisheria na zile za kimila zinazosimamia uendeshaji wa mabaraza haya.

Baada ya Baraza la Ardhi la Kijiji kutoa haki kwa watoto hawa yatima, maisha ya watoto hawa yamekuwa ya furaha tena na tabasamu limerudi kwenye maisha yao kutokana na kuwa huru kulitumia eneo ambalo nusura liporwe na wajanja wachache ambao walitaka kutumia unyonge wa watoto hawa kutofahamu sheria ya kutetea haki yao.

***"…Tunalishukuru Baraza letu kwa kusikiliza lalamiko letu na kulitolea maamuzi na hatimaye kunusuru eneo letu hivyo tutalitumia kwa kulima ili tuweze kujipatia chochote hasa chakula…."***

anasema Ndugu Jumanne Hamis ambaye ni baba yao mdogo na mlezi wa familia.

# VIJANA WANA NAFASI YA UJUMBE KATIKA MABARAZA YA VIJIJI NA KATA

*Na Tanzania Rural Women and Children Development Foundation (TARWOC)*



*Bi. Magreth Ng'ang'ani ambaye ni miongoni wa wajumbe wa Baraza la Kata ya Itunundu, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.*

Uzoefu unaonesha kuwa wengi wanaochaguliwa kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na ya Kata huwa ni Wazee kuliko vijana. Hii ni kutokana na ukweli kuwa katika mila na desturi za makabila mengi ya Tanzania Wazee wanaume ndio ambao husuluhisha migogoro kwenye ngazi ya familia, ukoo na hata ngazi za vijiji. Mtazamo huu umewafanya hata vijana walio wengi kutokuwa na hamasa ya kutumika kwenye Mabaraza wakiamini hizo ni kazi za Wazee zaidi.

Ingawa kutokana na mafunzo ya sheria za Ardhi na haki za ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini inayotolewa na taasisi za umma na zile za kiraia. Vijana wa kiume na kike wameanza kupata mwamko wa kushiriki kwenye vyombo vinavyofanya maamuzi ya kiutawala na kimaendeleo pamoja na vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kwa mfano, Bi. Magreth Ng'ang'ani mwenye umri wa miaka 27, mkazi wa Kijiji cha Kimande kata ya Itunundu, Wilaya ya Iringa ambaye aligombea nafasi ya ujumbe kwenye Baraza la Kata ya Itunundu na sasa ametumikia Baraza hilo kwa kipindi cha miaka 3. Bi. Magreth kwa kushirikiana na wajumbe wa Baraza hilo wamekuwa wakisuluhisha kesi mbalimbali ikiwemo ya ardhi.

Kwa mujibu wa Bi. Magreth, katika wajumbe wote wa Baraza hili la Kata yeye ndiye mjumbe kijana kuliko wote. Anaeleza zaidi kuwa wakati anaanza kuwa mjumbe ilikuwa ni ngumu sana kwa ushauri na mchango wake wa mawazo kukubalika na wajumbe Wazee kwasababu walimuona kuwa ni mtoto mdogo tena mwanamke ambaye kwa mila na desturi za kabila lao sio jambo la kawaida kwa mtoto wa kike au mwanamke kusema mbele ya wanaume na kueleweka kwa urahisi. Ila kadri siku zilivyozidi kusonga mbele walianza kumwelewa na kumuona kuwa wa msaada sana katika usuluhishi wa kesi mbalimbali kutokana na kuwapa mawazo mapya. Bi. Magreth alinukuliwa akisema kuwa;

*"…..nimekuwa nikikutana na changamoto nyingi kutoka kwa wanakijiji na vijana wenzangu kutokana na kazi hii ninayoifanya kama mjumbe wa kujitolea katika sababu niliamua mwenyewe nikachukua fomu nikaapishwa kama mjumbe wa Baraza wala sijakata tamaa ndio maana mpaka sasa naendelea… "*

Pamoja ya kuwa Bi. Magreth ni mjumbe wa Baraza la Kata lakini ana kisa chake na ndugu zake ambao walipitia misukosuko ya ardhi yao kuchukuliwa na Baba yao Mdogo baada ya Baba yao Mzazi kufariki. Anasema chanzo cha ardhi kuchukuliwa na Baba mdogo wao ni kwasababu familia yao ni ya watoto wa kike peke yake hivyo ilitafsirika kuwa Baba yetu hakuwa na mrithi wa mali zake ikiwa ni pamoja na ardhi. Anaongeza kuwa kwa wakati ule wakati Baba yao anafariki yeye na ndugu zake hakuweza kuchukua hatua yoyote ya kudai haki ya kurithi ardhi iliyoachwa na marehemu Baba yangu kwa sababu ya uelewa mdogo aliokuwa nao na vitisho kutoka kwa Baba mdogo.

Mwamko wa Bi. Magreth kudai haki yake na ndugu zake kumiliki ardhi pamoja na kuamua kusimama kidete kutetea haki za wasicha na wanawake wanaonyanyasika na mila kandamizi ulitokana na mafunzo ambayo yalikuwa yakitolewa na shirika la TARWOC la kuyajengea uwezo Mabaraza ya Kata katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ikiwa ni pamoja na Baraza la Kata ya Itunundu ambalo Bi. Magreth ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza hilo.

Baada ya elimu hiyo Bi. Magreth na ndugu zake walianza kusaka haki ya kupata na kumiliki mashamba ya marehemu Baba yao ambayo yalikuwa yamekwapuliwa na Baba yao mdogo. Walianza kutetea haki yao kwa kuweka pingamizi la upimaji wa eneo lililochukuliwa na Baba mdogo ambaye alitaka kujimilikisha kwa kutumia cheti cha hatimiliki ya kimila. Aliweza kuweka kizuizi kwamba eneo hilo lina mgogoro na kuomba kwa uongozi wa Kijiji eneo hilo lisipimwe. Pingamizi hilo liliweza kuzaa matunda kwake na dada zake kwani baba yao mdogo aliamua wakae kikao cha familia ili wapate suluhu ambayo iliishia kwa Bi. Magreth na dada zake kupata ardhi ya kumiliki baada ya Baba mdogo wao kurejesha ardhi hiyo kwao.

# NGUVU YA MWANAMKE NI UKOMBOZI WA FAMILIA

*Na Ujamaa Community Resource Team (UCRT)*



*Bi. Naishooki Konoro akiwa amesimama mbele ya nyumba yake anayojenga*

Waswahili wana msemo kuwa ukitaka kuikomboa jamii basi umwelimishe mwanamke, hii ni kwasababu katika jamii kuna mifano mingi inayosimulia namna ambavyo wanawake walisaidia familia na jamii zao katika nyakati ngumu za njaa, magonjwa pamoja na vita. Historia inawaonesha wanawake kuwa ni binadamu wanaojali, wanaojituma katika utendaji wa kazi, wenye huruma na wasiokata tamaa. Inafahamika kuwa wanawake ndio walezi wa familia kuliko wanaume hususani kwenye familia za Kiafrika ambazo wanaume huacha familia zao vijijini na kusafiri kwenda Mijini kutafuta kipato kwenye ajira rasmi na zisizo rasmi.

Katika jamii na familia nyingine wanawake ndio wanaosomesha watoto shule kwa kulipa ada, kununua sare za shule, vilevile ndio wanaogharamia huduma za afya, wanaohakikisha kuwa chakula kipo cha kutosheleza kwenye familia. Kuna wanawake pia ndio wanaojenga nyumba za kuishi wao na watoto wao na ndugu wengine na katika jamii ya sasa jambo hili limekuwa ni la kawaida sana kutokana na ugumu wa

maisha ambao umepelekea kila mtu kutafuta kipato kwajili ya familia bila kujali jinsia.

Katika kijiji cha Ngabolo, Wilayani Kiteto kuna mfano mzuri wa mwanamke ambaye anatekeleza majukumu ambayo yamejadiliwa hapo juu. Mwanamke huyu anaitwa Bi. Naishooki Konoro, ambaye ni Mama wa watoto 6. Bi. Naishooki pia ni mjumbe wa Baraza la Haki na Uongozi la Wanawake kijijini hapo. Bi. Naishooki alipata fursa ya kushiriki kwenye mafunzo ya haki za ardhi kwa wanawake yaliyotolewa na taasisi ya UCRT. Mara baada ya mafunzo hayo aliyopatiwa akiwa pamoja na wanawake wenzake, yeye alihamasika kupeleka maombi ya kupatiwa kiwanja kwenye Halmashauri ya Kijiji na kufanikiwa kupewa kiwanja chenye ukubwa wa mita 35 kwa 35.

Baada ya kupata eneo hilo Bi. Naishooki alianza kujipanga namna ya kuliendeleza eneo hilo kwa matumizi ambayo yangemnufaisha yeye na familia yake. Mwaka 2017 UCRT waliendesha zoezi la kuwasaidia wanawake kumiliki ardhi kwa kupata vyeti vya hatimiliki ya kimila, katika zoezi hili Bi. Naishooki alikuwa mmoja wa wanawake walionufaika;

***"…… nilifurahi sana kupatiwa hatimiliki ya kimila, ingawa sikuwa na uwezo wa kujenga ila nilijiambia lazima nikiendeleze kiwanja hiki…."***

anasema Bi. Naishooki

Katika kuhakikisha kuwa wanawake waliopata ardhi ya kumiliki wanazitumia ardhi zao kwa faida na manufaa, UCRT iliandaa mafunzo ya ujasiriamali na umuhimu wa kujiwekea akiba ya pesa kwenye VICOBA ambapo Bi. Naishooki naye ni mwanachama wa kikundi hicho. Bi. Naishooki ilibidi ashiriki kwenye biashara ndogo ndogo ili aweze kupata fedha ya kuchangia kwenye VICOBA. Biashara ambazo amekuwa akizifanya ni pamoja na kuuza mafuta ya kupikia na sabuni. Biashara hizi zimekuwa zikimsaidia uwezo wa kumudu kutoa hisa kila wiki kama sehemu ya kujiwekea pesa na kupata fursa ya kukopa mara tatu ya fedha alizowekeza kwa riba ndogo kwenye Kikoba hicho.

Mwaka 2020 Bi. Naishooki alipanga kulima mahindi hivyo alikopa pesa katika kikundi na kumuomba kijana wake wa kiume auze ng'ombe watano, pesa iliyopatikana aliwekeza kwenye kilimo na kupata faida ya shilingi Milioni mbili na laki saba (2,700,000/=) ambayo baada ya kuongeza faida alipata fedha ambayo ilimwezesha kuanza ujenzi wa nyumba yake ambayo inaonekana pichani hapo chini. Bi. Naishooki anasema kuwa;

***"…haikuwa rahisi kumshawishi kijana wangu anisaidie kwenye ujenzi kwa sababu mila na desturi zetu wamasai haziruhusu mwanamke kumiliki mali kwa jina lake bali kwa kupitia mume na watoto, lakini mwanangu alinielewa na kunisaidia kwa moyo wote, pia nashukuru serikali kwa kuleta sheria inayowapa watu wote haki sawa…"***

Bi. Naishooki amekuwa mfano wa kuigwa katika kijiji chake na vijiji vya jirani kutokana na maamuzi yake ya kuanza ujenzi wa Nyumba ya tofali jambo ambalo ni geni kwa jamii ya Wafugaji wa Kimaasai hasa linapofanywa na mwanamke ambaye kwa jamii kwa muda mrefu mwanamke huwa hahesabiki kuwa mtu wa maana au mwenye uwezo wa kufanya mambo makubwa kama ya ujenzi wa nyumba ya tofali. Bi. Naishooki amewapa hamasa wanawake wengine ambao wanamiliki viwanja kuanza kuviendeleza kwa sababu wengi wao walikuwa wanahofia kuwa ujenzi ni gharama sana. Sasa wamegundua kuwa ukiamua unajenga vizuri na kupata sehemu ya kuhifadhia chakula ambayo ni changamoto kubwa wanayokumbana nayo na mara nyingine hupelekea ukosefu wa chakula kutokana na uhaba wa maghala ndani ya kijiji. Watu wengi huishia kuuza mahindi yote na kuanza kununua tena ili tu kuepukana na usumbufu wa kutafuta sehemu ya kuyahifadhi.



# HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE NA MAENDELEO YA KIUCHUMI

*Na Wezesha Mwanamke (WEMWA)*



*Pichani ni Bi. Pili Ally na ng'ombe aliyemnunua shambani kwake*

Utetezi wa haki za ardhi kwa wanawake una faida gani? Ni kwanini wanawake wamiliki ardhi? Kuna faida gani mwanamke au wanawake wakimiliki ardhi? Haya ni baadhi ya maswali ambayo yamekuwa yakiibuka katika mijadala na mafunzo ya haki za ardhi kwa wanawake na makundi mengine ya kijamii kwenye maeneo mbalimbali nchini. Taasisi ya WEMWA ambayo inatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake katika Manispaa ya Singida nao wamekuwa wakikutana na maswali ya aina hii kutoka kwa wanaume, vijana na hata wanawake wenyewe.

Mradi huu unatekelezwa katika Manispaa hii ya Singida kutokana na wasichana na wanawake wengi kutokuwa na taarifa sahihi kuhusu haki zao za kumiliki ardhi na mali nyingine na namna ambavyo wanaweza kuitumia ardhi hii kukuza maendeleo na uchumi kwao na familia zao wenyewe na hata kijiji. Ni Dhahiri kuwa wanawake walio wengi kwenye maeneo ya mijini wanabaki nyuma kimaendeleo ingawa ndio wazalishaji wakubwa kwenye shughuli za kilimo na ufugaji.

Taasisi ya WEMWA imefanikiwa kuwasaidia wanawake ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakipitia manyanyaso ya kutokufahamu haki zao za ardhi. Kwa mfano Bi. Pili Ally Mnyiamba (38) mkazi wa kata ya Mungumaji ambaye ameolewa na ana watoto 6. Bi. Pili pia anatokea kwenye familia ya watoto 6 wakiwemo wanawake 2. Bi. Pili pamoja na mdogo wake wa kike walinyimwa urithi wa kumiliki ardhi ya wazazi wao kwasababu tu wao ni watoto wa kike na kwa mujibu wa mila na desturi zao hawaruhusiwi kurithi mali yoyote kutoka kwa wazazi. Kwa maana hiyo ni ndugu zao wa kiume tu ndio walioriithishwa ardhi na mali nyingine za familia.

Mnamo mwezi Agosti mwaka 2019, Bi. Pili alipata mafunzo juu ya Sheria za Ardhi na haki za ardhi kwa wanawake. Baada ya kupata mafunzo haya aliamua kwenda kuishirikisha familia yake kwa kuwapa elimu pamoja na kuwapelekea

majarida ili wajisomee wenyewe. Baada ya kujisomea, kujifunza na kujadiliana kwa muda mrefu ndugu wa kiume wa Bi. Pili akiwemo kaka yake mkubwa Ndugu Juma Ali alishawishika na akakubaliana na ombi la dada yao Bi. Pili na wakakubaliana kumpatia eneo lenye ukubwa wa ekari 2. Bi. Pili katika mahojiano yake alisema yafuatayo;

***''…naomba elimu zaidi iendelee kutolewa kwani ndio iliyochangia hata kaka zangu waridhie kunipatia sehemu ya eneo la familia japo kwa muda mrefu mila zetu zilikua zikipinga hili…''***

anasema Bi. Pili

Kwa sasa Bi. Pili anamiliki eneo lake na amefanikiwa kununua ngombe wa maziwa wa kisasa baada ya kuuza mazao ambayo alizalisha kutoka katika shamba alilopewa na kaka zake. Pia kwa kupitia vikundi vya kuweka na kukopa ambavyo waliunganishwa kupitia mtandao wa IR VICOBA ameweza kuongeza mtaji wake katika kilimo cha mahindi ambacho kinampatia faida ya kuendesha maisha yake na familia kwa ujumla.

# MAJUKWAA YA WANAWAKE DARAJA LA MATUMAINI VIJIJINI

*Na Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)*



*Bi. Getrude Sadick na Mchungaji Marko Abeli Nanyaro wakiwa katika eneo lenye mgogoro*

Umoja ni chachu ya maendeleo kwenye familia, ukoo, jamii, kijiji na hata katika taifa. Watu wengi waliofanikiwa kwenye kazi zao walikuwa na umoja, familia zilizofanikiwa kwenye mambo yao zilikuwa na umoja. Historia inatufundisha kuwa nchi za Afrika zilizowahi kupata uhuru kutoka kwenye ukoloni ni kwa sababu ya umoja ambao wapambania uhuru walikuwa nao. Historia inatukumbusha zaidi kuwa Taifa la Tanzania liliungana na nchi mbalimbali za Afrika ili kuwasaidia kujenga nguvu ya pamoja ya kuwaondoa wakoloni ambao walikuwa wamelowea katika nchi zao.

Hata katika lugha adhimu ya Kiswahili kuna methali na misemo mingi inayoonesha umuhimu wa kuwa na umoja kwenye maisha yetu ya kila siku ili tufanikiwe kwenye masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Methali na misemo hii ni pamoja "Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu", "kidole kimoja hakivunji chawa". Majukwaa ya wanawake yaliyoanzishwa na taasisi ya TAWLA katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru lengo kuu ni kuwaunganisha wanawake katika ngazi ya vijiji na kata katika kutetea haki za ardhi na haki nyingine za msingi kwa wanawake na watoto wa kike kwenye jamii ya Kimeru ambayo imegubikwa na mfumo dume unaowanyima wanawake fursa ya kuendelea kijamii na kiuchumi.

Majukwaa ya Wanawake yamekuwa msaada kwa wanawake kwa kushirikiana na kujadiliana kwa pamoja namna na mbinu za kupata fursa mbalimbali ikiwemo kujiendeleza kupitia ardhi zao na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kupitia majukwaa hayo, wanawake wameweza kunufaika kwa kupambania haki zao kwa kuchukua hatua baada ya kupata elimu ya haki za wanawake katika ardhi ikiwemo kutambua vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kufuata taratibu za sheria.

Kwa mfano mwaka 2016, Jukwaa la Wanawake katika Kata ya King'ori na Kijiji cha Muungano lilipatiwa mafunzo ya sheria za ardhi na haki za ardhi ambapo mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo alikuwa Bi. Monica Petro Ng'iti ambaye pia ni muumini katika Kanisa linaloongozwa na Mchungaji Marko Abeli Nanyaro. Baada ya mafunzo hayo Bi. Monica alimpa mrejesho Mchungaji Nanyaro kile walichofundishwa kuhusu haki za ardhi kwa wanawake.

Mchungaji Nanyaro alifahamu kuhusu habari za Mjane mmoja aliyefahamika kwa jina la Bi. Getrude Sadick ambaye ni Mkazi wa Kata ya Malula iliyopo Halmashauri ya Meru ambaye aliuziwa eneo kitapeli kwa maana kuwa eneo hilo hapo awali lilishauzwa kwa mtu mwingine. Mchungaji Nanyaro alimsaidia Bi. Getrude kupeleka shauri lake katika Baraza la Kata ya Malula ambapo baada ya kesi kusikilizwa uamuzi wa Baraza ulimpa ushindi Bi. Getrude. Baraza lilitoa amri kwamba arejeshewe eneo lake pamoja na gharama za usumbufu. Hata hivyo, kesi hiyo ilikatiwa rufaa katika Baraza la ardhi na nyumba la wilaya la Arusha, ambapo TAWLA inasimamia kesi hiyo ili kuhakikisha kwamba Bi. Getrude anapata haki yake.

# JAMII IBADILI MTAZAMO KUHUSU HAKI ZA WATOTO WA KIKE

*Na Tanzania Rural Women and Children Development Foundation (TARWOC)*



*Bi. Asha Msambwa akiwa mbele ya nyumba anayoijenga baada ya kupewa ardhi na wazazi wake*

Jamii nyingi za Kitanzania zina mtazamo kuwa haki pekee anayoweza kupata mtoto wa kike ni elimu na kufahamu kazi za ndani kama vile kufua, kuosha vyombo, kupika, kufanya usafi pamoja kuitunza familia. Ingawa kwa upande wa mtoto wa kiume pamoja na kupata elimu anatakiwa pia amilikishwe mali za familia kwa kuwa yeye ndio mrithi wa familia. Dhana hii na mfumo huu potofu umewaathiri sana watoto wengi wa kike kwa sababu hukosa haki ya kimsingi na ya halali ya kumiliki mali za wazazi wao kwa kigezo kimoja tu kuwa watoto hawa kike wataolewa na wataenda kukuta mali kwa waume zao.

Katika kupambana na mtazamo na dhana hii taasisi ya TARWOC imejikita katika kutoa elimu ya haki za ardhi kwa wanawake kwa makundi mbalimbali ya jamii kwenye vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Elimu hii imeweza kwa kiasi kikubwa kubadilisha mitazamo hasi kwa jamii hususani katika umiliki wa ardhi na mali nyingine kwa wanawake.

Taasisi hii pamoja na kutoa elimu kuhusu haki za ardhi kwa wanawake na makundi mengine kwenye jamii, imekuwa pia ikitoa elimu kuhusu namna ya kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye ngazi ya familia na ngazi ya kitongoji na kijiji

kwa ujumla wake. Mbinu ambazo zimekuwa zikitumika katika kutoa elimu hii ni pamoja na vipindi vya radio, matamasha ya michezo ya kuelimisha jamii, uanzishwaji wa majukwaa ya wanawake kwenye ngazi ya vijiji na kata. Kupitia mafunzo haya wazazi wengi wameweza kubadili mitazamo yao na kutambua kuwa watoto wa kike kama ilivyo kwa watoto wa kiume wana haki sawa katika kupata, kutumia na kumiliki mali za wazazi wao.

Mfano mzuri ni familia ya Mzee Hussen Msambwa ambayo ni familia yenye watoto 3 ambapo 2 kati yao ni wa kike na 1 ni wa kiume. Wazazi wa familia hii waliamua kugawa ardhi watoto wote bila kujali jinsia zao. Kila mtoto katika familia hii amepata ardhi ekari 1 na wana haki ya kufanya maendelezo yoyote katika ardhi kwa sababu kwa mujibu wa Baba yao mzazi hiyo ni mali yao. Mtoto mmojawapo katika familia hii ni Bi. Asha Hussen Msambwa mwenye umri wa miaka 23 ambaye baada ya kukadhiwa ardhi hiyo alianza kujenga nyumba ya vyumba vitatu ingawa bado haijakamilika. Ameweza kufikia hatua hiyo ya ujenzi kupitia shughuli mbalimbali za ujasiriamali ambazo amekuwa akizifanya kwa ajili ya kujiongezea kipato kama vile ushonaji. Bi. Aisha anaongeza kwa kusema kuwa;

***"… nina furaha sana kuwa miongoni mwa watoto wa kike wanaomiliki ardhi na ninawashukuru wazazi wangu kwa kunithamini na kunipa ardhi. Nawashauri na wazazi wengine waachane na mfumo dume, wawagawie ardhi watoto wao wa kike na wa kiume kwa kuwa watoto wote wana haki sawa…"***

# TABASAMU LILILOFIFISHWA LACHOMOZA TENA

*Na UMWEMA Group*



*Bi. Fatuma pamoja na shamba na nyumba yake ambavyo alirejeshewa kupitia Baraza la Kata*

Wataalamu wa masuala ya afya husema kuwa mwili wa binadamu ili uwe na afya imara unahitaji mjumuisho wa mambo mengi kama vile chakula, maji, matibabu, n.k. Lakini wataalamu wa Saikolojia husema kuwa tabasamu huimarisha afya ya akili na mwili kwa binadamu. Kwa maana hiyo binadamu anatakiwa ajitahidi muda mwingi uso wake uwe wa tabasamu wakati wote. Ingawa bahati mbaya maisha ya kila siku yanakuwa ni yenye changamoto na matatizo mengi hali inayomfanya kukosa tabasamu la kuimarisha afya ya mwili na akili yake.

Katika jamii na familia za Kitanzania kuna makundi mbalimbali ambayo tabasamu kwao limekuwa ni nadra sana kwasababu wamekuwa wakipitia matatizo ya mara kwa mara. Kundi mojawapo katika makundi haya ni Wajane. Wajane walio wengi wamekuwa wakinyanyasika kutokana na kunyimwa haki zao za msingi kutokana na mila na desturi za jamii husika. Kwa mfano tumeshuhudia Wajane ambao walinyang'anywa mali walizochuma na marehemu waume zao hivyo kulazimika kurudi kwa wazazi wao. Wakati mwingine Wajane hunyang'anywa hadi watoto na wake




na mashemeji zao kwa kigezo kuwa hawataweza kuwalea vizuri.

Nyakati nyingine vyombo vya utawala na utatuzi wa migogoro ya ardhi vimehusika katika kuwadhulumu na kuwanyima Wajane haki zao aidha kwa makusudi kabisa au kwa kutokufahamu kutokana na kutokupewa mafunzo ya sheria za ardhi na haki za ardhi. Kwa mfano Baraza la Kata ya Idibo, Wilayani Gairo ni moja ya Mabaraza ambayo toka kuanzishwa mwaka 2017 wajumbe wake hawakuwahi kujengewa uwezo kuhusu Sheria za Ardhi, haki za ardhi na taratibu za kuendesha mashauri yanayofunguliwa kwenye Baraza hilo. Matokeo yake haki za wananchi wengi wakiwemo wanawake wajane, yatima na wengineo wengi ziliminywa.

Mwaka 2019 taasisi ya UMWEMA iliyajengea uwezo Mabaraza 9 katika Wilaya ya Gairo likiwemo Baraza la Kata ya Idibo. Baraza hili sasa limekuwa ni tegemeo na kitovu cha utoaji wa haki kwa kupokea mashauri na kuyaendesha kwa haraka na bila upendeleo.

Mnamo tarehe 06/04/2020 Baraza la Kata lilipokea shauri la Mjane Bi. Fatuma Sued Mfaume mwenye umri wa miaka 68 dhidi ya Ndugu Dani Kilongora ambaye ni shemeji yake. Ndugu Dani alikuwa na dhamira ya kumdhulumu



Hukumu

Bi. Fatuma shamba na nyumba vyenye thamani ya shilingi Milioni Mbili na Laki Saba (2,700,000/=) kwa kudai kuwa hizo mali zote ni zake.

Baada ya shauri hilo kusikilizwa na mashahidi wa pande zote kutoa ushahidi, Baraza lilimpa Bi. Fatuma haki yake na kuamuru Ndugu Dani kuacha kutumia mali hizo na kuzirejesha kwa Bi. Fatuma. Baada ya kurejeshewa mali zake ambazo ni shamba na nyumba, Bi. Fatuma aliweza kulishukuru Baraza la Kata la Idibo kwa kupokea shauri lake, kulisikiliza na kutenda haki bila kuwa na upendeleo wa kijinsia hasa ukizingatia yeye ni mwanamke na jamii imekuwa na mtizamo tofauti na wanawake kuweza kumiliki mali za wenza wao pindi wanapofariki.

***''…..napenda kutoa shukrani zangu kwa uongozi wa Kijiji na lile Baraza kwa kunitendea haki bila kujali jinsia, leo nimepata mali zangu baada ya kudhulumiwa, kweli namshukuru Mungu sana. Nilisikia tu kwamba nikienda kwenye Baraza la Kata nitapata haki na kweli nimepata haki yangu sasa maisha yangu yatakuwa mazuri…"***


anasema Bi. Fatuma

# UMILIKI WA ARDHI WA PAMOJA NURU ANG'AVU UMASAINI

*Na Women Development for Science and Technology (WODSTA)*



*Ndugu Peter Songoyo na Mke wake Bi.Sayuni Songoyo*



*barua ya ombi la kupatiwa hati iliyoandikwa na Ndugu Peter Songoyo Mollel*

Sheria za Ardhi za mwaka 1999 zinatoa fursa ya mume na mke kumiliki ardhi kwa pamoja kwa majina yote ya mume na mke kuwemo kwenye hati ya umiliki wa ardhi pamoja na saini zao. Faida ya umiliki wa pamoja ni kuhakikisha kuwa wamiliki wote wawili wana haki sawa katika umiliki wa ardhi husika. Kwa maana nyingine maamuzi yoyote juu ya ardhi husika ni pamoja yaridhiwe na wote wawili.

Dhana hii ya umiliki wa pamoja sio nyepesi sana kueleweka hususani kwenye jamii za Kitanzania ambazo zinafuata mfumo dume katika kumiliki na kurithisha umiliki wa mali kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Uzoefu unaonesha kuwa wanaume ndio wamekuwa wagumu sana kukubali mfumo huu wa kumiliki ardhi kwa pamoja kwa hofu ya kuwa wanawake watakuwa na nguvu ya kimaamuzi katika ardhi hizo hivyo huchelea kukubali umiliki huo.

Taasisi ya WODSTA ambayo inatekeleza mradi wa haki za ardhi kwenye vijiji kadhaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ikitoa elimu hii kwa jamii za Wamaasai. Wanufaika wa mafunzo haya ni pamoja na wanawake, wazee wa mila, pamoja na wawakilishi wa viongozi ngazi ya kata na vijiji. Changamoto kubwa katika mafunzo haya ni ugumu wa wanaume kuelewa na kukubali kumiliki ardhi pamoja na wake zao.

Baada ya mafunzo hayo sehemu kubwa ya jamii imepata uelewa na kubadilika, moja mafanikio ni jamii kuhamasika na kuongezeka kwa kasi ya maombi ya hatimiliki za kimila na pia kumekuwepo na mitazamo chanya juu ya wanawake kuhusu haki ya kumiliki na kutumia ardhi kulingana na Sheria za ardhi Na. 4 na 5 ya mwaka 1999. Wanawake pia wamekuwa sehemu ya waliofanya maombi ya hatimiliki za kimila wao binafsi na kwa pamoja kati ya mume na mke.

Kwa mfano Ndugu Peter Songoyo Mollel ni mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo katika Kijiji cha Lemanda, Kata Oldonyosambu. Baada ya kupatiwa mafunzo hayo Ndugu Peter aliona umuhimu wa umiliki wa ardhi pamoja na mke wake Bi. Sayuni Peter Songoyo. Kwa sasa wapo kwenye mchakato wa kupata hati ya umiliki wa pamoja kupitia Halmashauri ya Kijiji na Halmashauri ya Wilaya.

# MFUMO DUME JINAMIZI LINALOWASUMBUA WAJANE

*Na Alpha Visible Community Development (AVCD)*





*Bi.Martha akiwa na mtoto wake Faustino Ngepa mbele ya nyumba yao*

Mfumo dume ni mfumo ambao unawapa wanaume nafasi ya kufanya maamuzi yote na ya muhimu kuanzia ngazi ya familia na ngazi zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mfumo huu umetamalaki kwenye jamii nyingi za Kitanzania kuanzia vijijini hadi mijini. Mfumo huu umejengeka katika misingi ya kuwa wanawake sio chochote wala lolote katika kufanya maamuzi. Kuna mifano mingi inayoonesha namna ambavyo wanawake na watoto wa Kike wameathiriwa na mifumo hii dume katika kila nyanja ya maisha kama vile elimu, afya, malezi, n.k.

Taasisi ya AVCD inatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake katika Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa. Wilaya hii ni moja ya wilaya ambazo mfumo dume bado ni tatizo linalowasumbua wanawake kwa kiasi kikubwa. Katika eneo la ardhi wanawake wamekosa haki ya kumiliki kutoka kwa wazazi wao kwasababu tu wao wana jinsia ya kike. Wajane nao wameathirika kwa kiasi kikubwa kwa kukosa haki zao kutokana na kudhulumiwa na ndugu za marehemu.

Moja ya mbinu ambayo inatumika na taasisi ya AVCD katika kutoa mafunzo ni pamoja na kuanzisha Jukwaa la wanawake katika vijiji mbalimbali wilayani Kilolo, mojawapo ya kijiji kinafahamika kama Mtitu. Jukwaa hili limepata mafunzo ya kutosha hivyo kuwasaidia wanawake ambao wamekuwa wanapitia changamoto za masuala ya ardhi kwenye familia zao.

Miongoni mwa wanawake walioguswa kwa karibu na Jukwaa hilo ni Mjane Bi. Martha Chaula ambaye alifiwa na mume wake mwezi Machi mwaka 2018 na kumuachia watoto 5. Ilipofika Januari 2019 ndugu wa marehemu mume wake wakiongozwa na Ndugu Bakari Ngepa ambaye ni mdogo wa marehemu walianza kudai mali za marehemu na baadae waliamua kuzichukua kwa nguvu baadhi ya mali hizo ikiwemo mifugo na vifaa vya kilimo. Vilevile, walichukua ardhi kwenye maeneo ambayo marehemu mume wake aliyatumia katika biashara zake za kufyatua tofali ambazo ziliingiza kipato kwenye familia.

Mnamo mwezi Agosti mwaka 2019 Bi. Martha aliripoti tatizo lake na shemeji zake kwenye Jukwaa la Wanawake katika Kijiji cha Mtitu kwa lengo la kupata msaada juu ya namna ya kutatua tatizo hilo ili apate haki yake ambayo aliiona namna inavyoporwa mchana kweupe. Kwa msaada wa Jukwaa hilo Bi. Martha alipatiwa utaratibu wa kufungua kesi kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji na baadae Baraza la Kata. Katika vyombo vyote hivyo Ndugu Bakari alikataa kuitikia wito na hivyo iliamuliwa shauri lipelekwe Mahakama ya Mwanzo. Kesi ilianza kusikilizwa na ilipofika Agosti 2020, Mahakama ilitoa hukumu kuwa Ndugu wa marehemu wanatakiwa kurejesha mali zote walizochukua na kutoendelea kutoa vitisho kwa mjane huyo na watoto wake. Baada ya hukumu hiyo kutoka na Bi. Martha kurejeshewa eneo lake alifurahi sana.

# HABARI KATIKA PICHA




*Kikundi cha wanawake cha kiuchumi na uelimishaji wa haki za ardhi katika Kata ya Mungumaji iliyopo Manispaa ya Singida*



*Wanawake wa Kijiji cha Wangama kilichopo Wilaya ya Iringa wakionesha hatimiliki zao za kimila*




*Bi.Happiness Mfinanga wa shirika la TAWLA akiwa katika mahojiano na waandishi wa habari katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani*




# HABARI KATIKA PICHA




*Maafisa mradi wa shirika la MPLC,Peter Kimath na Sakina Nyumayo wakiongea na Kikundi cha Mabinti Shujaa kilichopo kijiji cha Bonye Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro*



*Mwenyekiti wa Kijiji cha Ng'osi, Wilayani Kilolo ndugu Elioth Chengula akiongea na wanakijiji wake walipotembelewa na shirika la ICISO kwaajili ya kupatiwa elimu ya haki za ardhi na rasilimali nyinginezo kwa Wanawake*



*Wajumbe wa mkutano wa kufuatilia mpango kazi wa Mabaraza ya ardhi ya Vijiji katika Kata ya Sigino Wilayani Babati*

# ASASI ZINAZOTEKELEZA MRADI WA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE UNAOFADHILIWA NA FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY

IRINGA CIVIL SOCIETY ORGANIZATION (ICISO – UMBRELLA)
Email: iciso@yahoo.com
P.O.BOX 317, IRINGA

LAND RIGHTS RESEARCH AND RESOURCES INSTITUTE (LARRRI/HAKIARDHI)
Email: info@hakiardhi.or.tz
P.O.BOX 75885, DAR ES SALAAM.

ALPHA VISIBLE COMMUNITY DEVELOPMENT (AVCD)
Email: smtitu_adg_tz@yahoo.com
P.O.BOX 1002, IRINGA

COMMUNITY SUPPORT INITIATIVES – TANZANIA (COSITA)
Email: cositango@gmail.com
P.O.BOX 558 BABATI

WOMEN DEVELOPMENT FOR SCIENCE AND TECHNOLOGY (WODSTA)
Email: wodstatz@wodsta.or.tz
P.O.BOX 6584, ARUSHA

MOROGORO PARALEGAL CENTRE (MPLC)
Email: moroparalegal@gmail.com
P.O.BOX 6584, MOROGORO

TANZANIA RURAL WOMEN AND CHILDREN DEVELOPMENT FOUNDATION (TARWOC)
Email: tarwoc@hotmail.com
P.O.BOX 1056, IRINGA

UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM (UCRT)
Email: director@ujamaa-crt.or.tz
P.O.BOX 15111, ARUSHA

UMWEMA GROUP MOROGORO TRUST FUND
Email: umwemamorogoro@gmail.com
P.O.BOX 1272, MOROGORO

TANZANIA WOMEN LAWYERS ASSOCIATION (TAWLA)
Email: info@tawla.or.tz
P.O.BOX 996, ARUSHA

WEZESHA MWANAMKE (WEMWA)
Email: wezeshamwanamke@gmail.com
P.O.BOX 1686, SINGIDA

COMMUNITY ECONOMIC DEVELOPMENT AND SOCIAL TRANSFORMATION (CEDESOTA)
Email: cedesota2006@yahoo.com
P.O.BOX 13712, ARUSHA

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

fcs
FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
Facilitating Partnerships for Development